# Wavuvi watakiwa kuzingatia usafi Soko jipya la Malindi

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WAVUVI wanaotumia Soko jipya la Malindi ambalo limefunguliwa hivi karibuni wametakiwa kuzingatia usafi na kuhakikisha soko hilo linadumu kwa ajili ya kutimiza malengo yake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu, Masoud Ali Mohamed wakati alipotembelea soko hilo na kufanya mazungumzo na uongozi wa mkuu wa mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kuhusu mikakati ya kuliendesha soko hilo.

Alisema soko hilo limejengwa ikiwa ni sehemu ya ushirikiano na serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada (JICA) ambapo suala la usafi limezingatiwa katika kuendesha shughuli zake za biashara.

Aliongeza kuwa serikali ipo katika hatua za kutafuta watu au taasisi binafsi ambazo zitaendesha soko hilo kwa kuzingatia mahitaji ya usafi na kuliwezesha soko hilo kuwa la kisasa na kubaki katika ubora wake.

"Hili soko ni zawadi kutoka kwa wenzetu watu wa Japan ikiwa ni sehemu ya kutekeleza dhana ya uchumi wa buluu kwa wafanyabiashara kuendesha shughuli zao kisasa, hivyo tupo katika kuweka mikakati ya kulitunza," alisema.

Mapema Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Mustafa Kitwana aliwataka wafanyabiashara pamoja na wavuvi wanaolitumia soko hilo kuhakikisha wanazingatia usafi wakati serikali ya mkoa ikiwa katika juhudi za kutafuta watu watakaoliendesha.

"Kwa upande wa serikali ya mkoa tumejipanga kuzingatia usafi katika soko hili. Wachuuzi wa samaki wanatakiwa kutumia maeneo maalumu yaliyowekwa kwa ajili ya kufanya usafi," alisema.

Katibu Mkuu, Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Aboud Suleiman Jumbe aliwataka wavuvi kuhakikisha wanalitumia soko hilo kwa kupeleka samaki wanaozingatia viwango waliovuliwa kwa kufuata uvuvi unaokubalika kwa mujibu wa sheria ya uvuvi.

"Wapo maofisa wetu wa uvuvi ambao miongoni mwa kazi zao ni kufuatilia maendeleo ya uvuvi pamoja na kujua aina ya uvuvi unaotumiwa kwa ajili ya kuvua samaki kwa mujibu wa sheria za uvuvi ambapo nyavu zenye macho madogo zinazonasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula hatuzitaki," alisema.

Baadhi ya wavuvi na wachuuzi wa samaki katika soko jipya wameipongeza serikali ya Zanzibar kupitia serikali ya Japan kwa kujenga soko la kisasa lenye mahitaji yanayokwenda na wakati.

"Hili soko ni la kisasa bora ambapo tunaahidi kulitunza kwa kuzingatia usafi ambapo tumejipanga pia kuhakikisha ulinzi wa vyombo vya usafiri unaimarishwa ili kuepuka matukio ya wizi," alisema Haji Faki ambaye ni mchuuzi katika soko hilo.

Tayari wavuvi na wachuuzi wa samaki wameanza kulitumia soko hilo huku likiendesha minada ya samaki kwa wavuvi wanaotoka sehemu mbalimbali ambapo wafanyabiashara wengi ikiwemo wanawake wamekuwa wakifanya shughuli zao.

CS CamScanner

HABARI LEO UK 19

*



*Wachuuzi na wafanyabiashara wa samaki wakinunua kitoweo hicho katika soko jipya la samaki lililozinduliwa hivi karibuni na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, eneo la Bandari ya Malindi, Unguja juzi. Soko hilo limejengwa kwa ufadhili wa serikali ya Japan. (Picha na Khatib Suleiman).*

# Wafugaji yatumieni majosho ya serikali

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

SERIKALI imewataka wafugaji kupeleka mifugo yao kwenye majosho ya serikali yaliyojengwa maeneo mbalimbali ili kuikinga mifugo dhidi ya magonjwa yaliyotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana na jamii ya wafugaji katika Kijiji cha Machenje wilayani Kongwa jijini Dodoma, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Chilo aliwataka wafugaji watunze mazingira ili kuruhusu majani kuota.

Katika ziara hiyo alishuhudia namna ng'ombe wanavyopita kwenye majosho na kupata fursa ya kukagua miradi mbalimbali ikiwamo uchimbaji wa visima kwenye maeneo ya vijiji vya Mtanana, Chigwingwili, Soiti, Ndalibo, Ugogoni, Machenje, Nguji, Ibwaga na Chitomolo.

Akizungumza na wananchi hao, Chilo aliwataka wale wanaomiliki mifugo ya miguu minne, wahakikishe wanaipeleka kwenye majosho hayo.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji waliofika kuogesha mifugo, Abdi Juma aliishukuru serikali kwa kuwaletea huduma hiyo ya majosho ambayo itaondoa hasara waliyokuwa wakiipata ikiwamo vifo vya mifugo.

"Tumekuwa tukipoteza mifugo kwa kufa kutokana na mazingira kuwa jangwa, kwa hiyo miradi hii ikiwamo ya sehemu ya kunywesha mifugo, majosho ya kuwakinga na magonjwa inasaidia kuondokana na tatizo hili," Juma alisema.

Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kongwa ulizinduliwa mwaka 2021 na unatekelezwa kwa miaka mitatu hadi mwakani na takribani wafugaji na wakulima zaidi ya 45,000 wanatarajiwa kunufaika.